4th COMMUNITY OF PRACTICE FOR LEARNER-CENTRED EDUCATION

Dec 2011 CONFERENCE

UBORESHAJI WA MAFUNZO YA UALIMU:

ANITHA KIHIYO

SHULE YA MAZOEZI KIGURUNYEMBE

UBORESHAJI WA MAFUNZO YA UALIMU

UTANGULIZI.

Taaluma ya ualimu ni msingi/mhimili mkubwa katika Taifa lolote lile. Katika taaluma hii ya ualimu huwezesha Taifa kuwa na wataalamu mbalimbali kama vile madaktari, engineers, wahasibu, wanasheria, wajenzi n.k. Hivyo basi mwalimu ambaye ni mtaalamu anapaswa kuwa na uwezo wa kufanya taaluma yake kuwa chachu ya kuleta maendeleo katika elimu na kama mtu yoyote atashindwa kufanya au kuonesha uwezo wake basi huyo si mtaalamu na anapaswa kuondolewa katika taaluma hiyo.

Uboreshaji wa matunzo ya ualimu hayana budi kuzingatia taaluma za walimu wanaozalishwa kila kukicha katika vyuo mbalimbali vya ualimu nchini. Serikali inapaswa kutambua kuwa taaluma ya ualimu ikiboreshwa basi itakuwa imejijengea misingi iliyo imara katika maendeleo. Hakuna Taifa lililoendelea bila kuwa na wasomi. Pia ifahamike kuwa kila Taifa ulimwenguni linapendelea kutoa elimu bora katika maeneo yote ya elimu ilikuwezesha na kuzalisha Taifa lililo na watu walioelimika waliojaa maarifa na yanayowezesha kukabiliana na changamoto za kiulimwengu.

Uboreshaji wa mafunzo ya Ualimu na vipengele vyake.

1. ***Taaluma ya Ualimu Yenyewe.***

Taaluma ya Ualimu bado inasuasua kwani bado haijafahamika kama ni kweli ni taaluma au la. Walimu walio wengi huingia katika unyago wa ualimu kwa sababu wanakuwa wamekosa nafasi katika taaluma nyingine. Myra (1980) anasema kwamba “Teaching was viewed not as a career but as a temporary employment many of those who entered teaching were teenagers who taught for any a year or two. Others were of dubious character and a number of teachers fired for drinking”.

Hivyo basi kutokana na kutokutambulika vizuri kwa taaluma hii wengi huingia na kutoka na kutafuta kazi zingine. Katika kufanikisha hili ifahamike kuwa taaluma ya ualimu ni nyenzo kuu katika kumwezesha mwanafunzi kupata maarifa stahiki na kumjengea uwezo wa kupambanua mambo mbalimbali katika maisha kwa ujumla. Kuwezesha hilo mwalimu anapaswa kuandaliwa vya kutosha na pia apewe nyenzo mbalimbali katika ufundishaji wake. Sifa za mwalimu zifahamike na zilingane na

maadili pamoja na miiko ya ualimu. Mwalimu anapaswa kuwa na ueledi wa kutosha katika fani hiyo na hii itamsaidia katika kukabiliana na changamoto mbalimbali katika kazi yake.

Ili taaluma ya ualimu itambulike kuwa ni taaluma kama nyingine inapaswa kuwa au kufikia viwango vifuatavyo.

Kwanza kabisa, lazima kuwe na mafunzo dhahiri katika elimu ya ualimu. Mwandishi Abert Ozigi wa Nigeria (1980) alisema kuwa nanukuu "For a person to qualify as a professional he must undergone a specialized standard in a recognized institution". Sambamba na mwandishi huyo kuna mwandishi mwingine Myra (1980) aliongeza kuwa "Preparation of an induction into the profession is provided through a protracted preparation program; usually in a professional school on a college or university campus". Hivyo basi, katika kuboresha mafunzo ya ualimu hatuna budi kuhakikisha kuwa kila mwalimu anapaswa kupata mafunzo stahiki na yenye viwango vinavyotakiwa. Mafunzo hayo pia yasimamiwe vizuri na wakufunzi wanaopaswa kuwa mahiri.

Pili, maadili ya kazi, kwa ujumla maadili ya kazi ya ualimu hayatofautiani na taaluma zingine. Katika uboreshaji wa mafunzo ya ualimu ni lazima izingatie maadili. Walimu waelezwe ni vitu gani wanapaswa kufanya na vitu gani wanapaswa kuachana navyo hasa katika makuzi na malezi ya wanafunzi. Katika hili pia mwalimu anapaswa kufahamu kuwa nawajibu mkubwa kwa wanafunzi hasa katika suala la ufundishaji.

Tatu, uwepo wa vifaa na zana kwa ajili ya kufundishia. Hii pia hufanya taaluma ya ualimu kuonekana kuwa taaluma halisi. Kukiwa na vifaa vya kutosha katika ufundishaji, mwanafunzi huelewa vizuri. Umahiri wa mwalimu katika utumizi wa vifaa hivi humjenga mwanafunzi uwezo wa kuelewa na hata kutenda kwa ufanisi.

Katika kuwezesha haya Serikali haina budi kuimarisha mafunzo ya ualimu kwa kuangalia vigezo mbalimbali vinavyoweza kuinua elimu nchini.

2. Uimasrishaji wa maadalizi ya ualimu.

Maandalizi ya ualimu huanzia vyuoni ambapo walimu hupata mafunzo mbalimbali yahusuyo malezi, makuzi na ufundishaji kwa wanafunzi. Huelekezwa njia mbalimbali ambazo huwa nyenzo kuu katika ufundishaji na ujifunzaji.

- Mafunzo ya ualimu au maandalizi ya ualimu huchukua miaka miwili kwa Diploma na Cheti. Katika miaka miwili hiyo walimu wanafunzi hupata maarifa mbalimbali jinsi ya kukabiliana na changamoto mashuleni.
- Walimu wanafunzi pia hupewa muda kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo katika kupima ni jinsi gani watakavyoweza kutoa maarifa yao na kuwapa wanafunzi ambao ni walengwa. Katika muda huo wote huwa wanafuatiliwa na kupimwa na wakufunzi wao. Na muda unapoisha hurudi vyuoni.

Katika kuimarisha maandalizi ya ualimu, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi haina budi kutilia na kuangalia sekta ya ualimu kwa umakini sana bila kukurupuka.
Kwanza kabisa, wanapaswa kuangalia upya sifa za mwalimu tarajali kabla hajajiunga na Chuo. Sifa zake zinapaswa zilingane na za taaluma zingine, pia sifa zake katika ufaulu ziwe za juu na si za chini kama ilivyo sasa katika kufanya hivyo walimu watakuwa ni bora. Kama Wizara husika itazingatia vigezo katika uchaguzi wa walimu itaweza kuleta tija katika mafunzo hayo. Pia waelewe kuwa mwalimu ana sifa zake akikosa sifa moja basi huyo hajakamilika kuwa mwalimu.

Mabadiliko ya mitaala, mabadiliko hayana budi kutokea na pia yanapaswa kuendana na wakati. Lakini pia yanapaswa kuendana na mahitaji ya jamii au Taifa husika. Mabadiliko hayo pia yanapaswa kuangalia ni nini kinaweza kutokea baadae. Pia mabadiliko hayo yaende sambamba na uwezo wa vitabu vya masomo husika ambayo kwa namna moja au nyingine yameongezwa au kusahihishwa katika mtaala. Kwa mfano, kuna masomo mengi yanaweza yakaongezwa, hivyo Wizara haina budi kuandaa mwongozo kwa ajili ya masomo mapya.

Kwa ujumla mtaala wa elimu unatakiwa kuendana na hali halisi ya maisha wanayoishi wanafunzi na hii itamsaidia mwanafunzi kutumia maarifa na ujuzi alioupata shuleni na kuhusianisha na maisha ya kila siku katika kuimarisha maandalizi ya walimu. Serikali haina budi kutilia mkazo mabadiliko ya mitaala kwa mfano, kwa sasa mtaala unalenga zaidi ushirikishwaji wa mwanafunzi mwenyewe katika ujifunzaji. Hivyo basi walimu wazingatie mabadiliko hayo katika ufundishaji wao. Kwa kitaalamu mabadiliko hayo ya elimu yanaitwa “Change of Paradigm in Education” yaani “Mhamo wa Ruaza”. Mabadiliko haya

yanamlenga mwanafunzi kuwa ndiye chanzo cha maarifa na mwalimu kubaki kuwa muezeshaji wa tendo la ufundishaji na ujifunzaji. "In that sense the current school curricular in Tazania are competence – based and are formulated within the constructivist paradigm. Thus were expecting to shift school learning and teaching to comply with the new paradigm" Noah Mtana.

- ***Sifa za kujiunga na mafunzo ya ualimu vyuoni.***

Mwalimu bora na makini ni yule mweye sifa nzuri na anayekubalika na wanafunzi wake. Katika sekta ya elimu sifa za mwalimu zimekuwa hazizingatiwi na hatma yake kuleta na kuzalisha walimu wasio kuwa na sifa. Ili kuimarisha mafunzo ya ualimu, Serikali haina budi kuangalia upya sifa za mwalimu anayeomba kujiunga na mafunzo hayo. Vigezo vya Principal mmoja na subsidiary moja havikizi viwango bora vya mwalimu. Taaluma ya ualimu haina budi kupewa kipaumbele kwani ndio sekta mama. Katika kufanya hivyo ubora wa elimu utakuwa wa hali ya juu kwani kila mwalimu atakuwa mahiri kutokana na kiwango cha elimu na sifa aliyonayo.

- ***Muda wa Mafunzo.***

Muda wa mafunzo kwa walimu kama nilivyoelezea awali ni miaka miwili kwa ngazi ya Stashahada na miaka miwili kwa ngazi ya Cheti. Sifa mojawapo na mafunzo hayo ni lazima yawe ya muda mrefu. Kwanini muda mrefu?

Kipengele cha muda mrefu ni cha msingi sana kwani ni pale mwalimu anapopata maarifa ya kutosha ambayo yatamjengea uwezo wa kutambua ni nini afanye kwa wanafunzi wake, na akishafanya anategemea nini kwa wanafunzi anaowafundisha.

Mwalimu tarajali anapokuwa katika mafunzo kwa muda mrefu pia humwezesha kujua na kutumia mbinu mbalimbali za ujifunzaji na ufundishaji na hivyo kupatia umahiri katika ufundishaji. Pia humjengea kuwa na uwezo wa kupanua upeo na uelewa, kuinua na kukuza hali ya kujiamini na kuwa na udadisi juu ya mambo mbalimbali. Ieleweke kuwa uzoefu wa kufanya kitu muda mrefu huwa ni bora zaidi ya ule wa muda mfupi.

Wataalamu wa mambo ya jamii wanaamini kuwa "Experience is a good teacher". Mwandishi Myra anaelezea yafuatayo katika muda wa mafunzo ya mwalimu "Teaching profession has short preparation

time for becoming a teacher; lack of influence over certification and the entry of others into the field; weak policing of the ranks for incompetence and an inadequate base of specialized knowledge. Also claimed that; “teaching has not yet achieved professional status. Teachers; they say, go through a relatively short preparation period – shorter than for some of the skilled trades. They exercise little influence over certification; entry standards or teacher preparation”

Hivyo basi katika uimarishaji wa mafunzo hatuna budi kubadilika na kuangalia ubora wa mafunzo ya ualimu. Kwa mfano Crash Programme kwa walimu inarudisha nyuma ubora wa elimu nchini, kwani walimu waliopitia mafunzo hayo hawakuiva ipasavyo. Kwa kuzingatia hili Wizara ya Elimu haina budi kubadili mfumo wa elimu ili kuzalisha walimu walio bora.

Pia walimu makazini ambao hawajapitia mafunzo hawana budi kupatiwa mafunzo ya ualimu kwa muda stahiki. Mwandishi Albert Ozigi (1979) anasema kuwa “there is a need for regular inservice training programmes for training and retraining primary school teachers with a view to their professional improvement and upgrading. If this done then those engaged in teaching at all level can key some crime to be professional teachers”. Hivyo tukizingatia vigezo tutaweza kukomesha tabia iliyojengeka kuwa ualimu ni kazi ambayo mtu yoyote hata asiye na ujuzi wa taaluma hiyo kuweza kufanya kazi hiyo.

CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI TAALUMA YA UALIMU.

Pamoja na kuwepo nyenzo mbalimbali za kuimarisha na kuboresha taaluma au sekta ya elimu bado kuna changamoto mbalimbali. Changamoto hizi kwa namna moja au nyingine zinashusha kiwango cha utaji wa elimu.

Taaluma.

Kutokuwepo na bodi inayotetea maslahi ya walimu kwa namna moja au nyingine ni changamoto kubwa ambayo inafanya walimu kutokuwa na mtetezi imara katika kazi na maslahi kwa ujumla. Pia kutokuwa na bodi inasababisha walimu kutokuwa na maadili au kutofuata maandi ya kazi. “There is a need to have a recognizedboard that can control our profession. Boar should be introduced and organized into associations. Myra 1980 said “the professions which within board limits of social accountability; are granted autonomy in a control of the actual work of the profession and the

conditions which surround it. (admissions, educational standards; examination and licensing, career line; ethical and performance standards). If some standards are set then teaching professional will be valued like other professions. Teaching left in air because it lacks accountability and autonomy. By valuing it will limit teachers to runaway". Bodi ya ualimu ikiundwa itaweza kutatua matatizo mbalimbali ya walimu na maadili kwa ujumla yatazingatiwa.

Maadili ya kazi kwa walimu.

Walimu walio wengi hawafuati miiko ya kazi na hii inapelekea kupunguza ubora wa kazi yenyewe. Kwa mfano walimu hujiingiza katika ulevi, wizi wa mitihani, uhuni, uzembe, rushwa na mienendo mingine mingi. Kwa kufanya hivyo hadhi ya taaluma hupungua na kudharaulika na jamii. Myra 1980 "Cocles of conduct and ethics in education system are not mostly oserved by teachers and this tends teaching not be recognized as a profession". Pia Ablert Ozigi anaongeza kuwa "it should be true to say that many of our practicing teachers are sometimes guilty of unprofessional conduct (such as illegitimate sexual relations with their students' leakage of examinations deliberate using of and misleading students for selfish and, total neglect of work in and students.

Uhaba wa zana au vitendea kazi kwa ajili ya kufundishia na kujifunzia.

Ni dhahiri kuwa mkulima hawezi kwenda shambani mikopo mitupu, ni lazima awe na jembe, panga, shoka n.k. na hii itamsaidia kufanya kazi vizuri, vivyo hivyo kwa mwalimu na mwanafunzi, mwalimu hawezi kufundisha akaeleweka bila kuwa na maarifa ambayo anayapata kutoka katika vitabu n.k. na pia hawezi kueleweka bila kuwa na chaki na kalamu. Pia wanafunzi hujifunza na kuelewa kwa kuona, kusikia na kutenda jambo. Hivyo kwa kuona na kufanya kunahitaji vitendea kazi ili waweze kutenda. Pia sambamba na hilo mwalimu hana budi kufahamu matumizi ya vitendea kazi. Kuna tatizo kubwa kuwa vifaa vinaweza kuwepo lakini mwalimu akashindwa kutumia kifaa hicho. Walimu hawana budi wa kukubali kujifunza juu ya matumizi mbalimbali ya zana. Ozigi anasema kuwa "to be an effective practitioner, a professions must not only possess the knowledge and skills of his trade but also the necessary tools, the standards of the equipment and teaching facilities".

Mishahara.

Hii ni changamoto nyingine inayoikabili sekta ya elimu. Malipo ya mishahara kwa walimu hailingani na taaluma nyingine na hii inapelekea walimu kutokutimiza wajibu wao. Wengi hujikita katika kufanya kazi zingine nje ya kazi ya ualimu; walimu wengine hujiingiza katika utoro na utendaji kazi huwa hafifu na hii inapelekea wanafunzi kufeli katika mitihani yao nah ii huwashangaza wengi na kutafuta mchawi. Mchawi wa mwalimu ni mshahara endapo atalipwa vizuri atafanya kazi yake kwa kujituma na kujitolea. *Myra (1980) "according to a recent pool, more than half of today's' teachers say they have seriously considered leaving teaching because of poor salary and poor working conditions. And an adequate salary and sense of pride and self-worth that comes from doing an important job well and knowing that other' respect your competence. Financial well being and community respect usually go hand in hand with professional status.*

Serikali ichukulie uzito swala zima la mishahara kwa walimu ili ufanisi wa kazi uongezeke.

Mafunzo ya walimu kazini

Mafunzo ya Walimu kazini (Professional Development) kutokuwepo na matunzo ya mara kwa mara kwa walimu kazini pia ni kikwazo kwa taaluma ya ualimu. Mwalimu anapopata mafunzo ya mara kwa mara humwezesha kujifunza na kubaini mbinu mpya za kufundisha na kwenda na wakati uliopo.

Maadili ya wanafunzi.

Wanafunzi walio wengi hawana maadili ya kutosha nah ii kupelekea taaluma ya ualimu kupata wakati mgumu katika makuzi na malezi ya wanachuo. Kwa mfano shule za mijini zinakabiliwa na tatizo kubwa la maadili mabaya kwa wanafunzi kwa asilimia kubwa.

Uwezo wa walimu katika uwasilishaji wa mada.

Walimu walio wengi hawawezi kuwasilisha mada huenda ikasababishwa na kutokuwa na uwezo wa kutosha katika kutoa maarifa aliyonayo na kumpatia mwanafunzi. Kwa mfano katika hii dhana ya "Competence Based Curriculum" walimu walio wengi wanashindwa kutumia ujuzi katika kuwawezesha wanafunzi kuelewa. Bado mwalimu anatumika kama chanzo cha maarifa pekee badala ya mwanafunzi

kuwa mshirikishwaji wa kwanza. Kwa sababu hiyo, mwalimu hushindwa kukabiliana na changamoto zilizopo mashuleni na jamii inayowazunguka.

Mwalimu mbunifu.

Walimu walio wengi si wabunifu wamekuwa ni watu kukaririsha maarifa kwa wanafunzi wao. Ifahamike kuwa elimu anayoipata mwalimu ni lazima imsaidie kuibua udadisi na kuchochea maswali kwa wanafunzi wake. Hii ni changamoto nzito ambayo inapaswa kutazamwa kwa macho mawili la sivyo elimu itadumaa au kurudishwa nyuma. Mwalimu ni lazima akubali kujifunza na kufikiri kwani kwa kufanya hivyo itamsaidia kubuni njia mbalimbali za ufundishaji na ujifunzaji na hivyo kukabiliana na changamoto mbalimbali za elimu. Ubunifu huo pia lazima uendane na mahitaji na matakwa ya mtaala unaoendana na ujuzi yaani "Competence Based Curriculum".

MIKAKATI KATIKA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO.

Kutokana na changamoto nyingi zinazoikabili taaluma ya ualimu hatuna budi kuwa na mikakati madhubuti ili kuifanya taaluma ya ualimu kuwa na hadhi na kutambulika kama taaluma zingine.

Njia ambazo zinaweza kukabiliana na changamoto hizo ni hizi zifuatazo:

- Mishahara ya walimu iongezwe kulingana na elimu ya mwalimu. Lakini si elimu aliyonayo mwalimu bali iongezwe kulingana na kazi kubwa aliyonayo mwalimu. Ikumbukwe kwamba mwalimu ndiye mlezi wa mwanafunzi, kuna Mwanasociologia Philipa alisema kwamba, mwanafunzi hukaa muda mrefu shuleni kuliko nyumbani au mahali popote na hapo mwalimu huwa na kazi kubwa katika kuangalia mienendo na tabia ya mwanafunzi huyo.
- **Vifaa vyakujifunzia na kufundishia.**

Uwepo wa zana za kujifunzia na kufundishia huleta tija katika swala zima la ujifunzaji na ufundishaji. Wizara husika na Serikali kwa upande mwingine haina budi kuzingatia hilo kwa umakini sana. Ozigi 1979 anasema kuwa "A truly professional teacher cannot tech effectively unless he has range of equipments at his disposal just as surgeon cannot perform certain operation unless he has a range basic equipment at his disposal". Kazi ya ualimu haiwezi kutimizza malengo yake bila kuwa na vifaa

hiyo, Serikali na Wizara husika zifanye kazi ya ziada katika kuhakikisha vitendea kazi vinakuwepo mashuleni.

- Bodi iundwe ili iweze kutetea maslahi ya mwalimu na kuleta maendeleo katika sekta ya ualimu.
- Maadili ya ualimu yafuatwe na yasibezwe na watu ambao wanaingilia kazi au taaluma hii wakidhani ni taaluma ya wahuni. Vigezo vya mwalimu havina budi kutambulika na kueleweka baina ya walimu, miiko ya mwalimu iainishwe kwa mapana na marefu. Kwa kufanya hivyo tutaweza kukabiliana na changamoto hiyo.
- Mafunzo ya walimu kazini yawe ya mara kwa mara ili walimu hao waendane na mabadiliko ya mitaala na kuweza kukabiliana na changamoto mbalimbali za elimu nchini.
- Mafunzo ya walimu yazingatie muda dhahiri na si leo mwaka mmoja mafunzoni n.k. bali yazingatie sifa ya taaluma yenyewe. Wizara isimamie vema swala la muda wa mafunzo na si kwa kupelekwa pelekwa na siasa. Sekta ya elimu ni nyenzo muhimu sana kuliko sekta nyingine. Kwa kuzingatia hilo tutaweza kukabiliana na changamoto ya mafunzo ya ualimu.
- Katika kukabiliana na swala la maadili ya wanafunzi hatuna budi kuishirikisha jamii katika kuhakikisha kuwa wanafunzi wetu wanakuwa katika mwenendo mzuri. Kwa nini jamii? Jamii inahusika moja kwa moja kuishi sehemu ambayo mwanafunzi, mwalimu na mzazi wanaishi pamoja. Hivyo ni rahisi kuelekezana na kuonyana.
- Mwalimu ni benki ambayo haishiwi maarifa, hivyo mwalimu hana budi kuwa mbunifu ili aweze kukabiliana na changamoto z kila siku katika ufundishaji wake.
- Mwalimu hana budi kujua njia mbalimbali katika uwasilishaji wa mada yoyote ile kwa wanafunzi wake. Kwa kufanya hivyo mwanafunzi ataelewa kwa urahisi zaidi hata kuweza kufanya na kutenda bila usimamizi wa mwalimu.

HITIMISHO.

Taaluma ya ualimu ili iweze kuimarishwa inahitaji msaada mkubwa kutoka kwa wadau na wahisani wa elimu. Bila kuwa na msaada huo, sekta au taaluma ya ualimu itapoteza mwelekeo. Changamoto zinazoikabili sekta hii zikiboreshwa na kufanyiwa kazi basi itasaidia taaluma kusonga mbele, na hii itaifanya taaluma hii kuheshimiwa na watu wote kwani **“ELIMU NDIO UFUNGUO WA MAISHA ASIYEKUWA NA UFUNGUO HUO BASI HAWEZI KUFUNGUA MLANGO”.**